SHULE YA SEKONDARI MSUVA,
S.L.P 141,
Barua pepe. msuvasecondari@gmail.com
Mob.................................
Tarehe. ...........................

Kumb. Na.........................................
Jina la Mwanafunzi ...........................................
S.L.P .........................................
SIKONGE.

**YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MSUVA, WILAYA YA SIKONGE, MKOA WA TABORA MWAKA 20……**

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka ……………… **Shule ya Sekondari Msuva** ipo umbali wa **KM 28** Kusini mwa Halmashauri ya **WILAYA YA SIKONGE.**

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe ………………......... unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ………………...na mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………….ndani ya siku saba.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za shule

a) Sare za shule hii ni

**WAVULANA.**

i. Suruali 2 tetroni bluu nzito (dark blue)
ii. Shati 2 tetroni nyeupe mikono mifupi na mfuko mmoja
iii. Tai ndefu rangi ya suruali
iv. Viatu vyeusi vya ngozi
v. Soksi nyeupe au kahawia
vi. Sweta dark blue

**WASICHANA.**

i. Sketi 2 tetroni bluu nzito (dark blue)
ii. Shati 2 tetroni nyeupe mikono mifupi na mfuko mmoja
iii. Tai ndefu ya rangi ya sketi
iv. Viatu vyeusi vya ngozi visigino vifupi
v. Soksi nyeupe ndefu
vi. Sweta dark blue

b) Rangi ya Hijabu ifanane na sare ya shule hii.

c) Sare ya michezo kwa shule hii ni

**WAVULANA**

i. Suruali nyeusi ya tetroni
ii. Bukta ya Dark blue
iii. Viatu vya raba.
iv. T –sheti ya shule

**WASICHANA**

i. Sketi nyeusi tetroni
ii. T – sheti ya shule

iii. Bukta yenye mpira chini dark blue
iv. Viatu vya raba.

2.2 Daftari, kalamu na mkebe wa hesabu.

2.3 Chakula cha wanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.

2.4 Nauli ya wanafunzi wa bweni kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo, godoro na vifaa vya malazi.

2.5 Mahitaji mengine ya kibinadamu (kama yapo yatajwe).

### 3.0 Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;

c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);

d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;

e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na

i) Kutunza mali za umma.

3.2 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au kusimamishwa Shule

a) Wizi.

b) Uasherati na ushoga.

c) Ubakaji.

d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.

e) Kupigana au kupiga.

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

g) Kudharau Bendera ya Taifa.

h) Kuwa mjamzito / kupata mimba.

h) Kuoa au kuolewa.

i) Kutoa mimba.

j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

k) Kukataa adhabu kwa makusudi.

l) Kuwa na simu ya mkononi.

**4.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi**

a) Medical Examination Form' ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

*Phillipo J. Mziray*
**MKUU WA SHULE**

# WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI .
# SHULE YA SEKONDARI MSUVA.

## KUJIANDIKISHA
*(Ijazwe kikamilifu na kukabidhi ofisini)*

1. Jina kamili la mwanfunzi ..............................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa ......................................................................
3. Mahali ulipozaliwa (wilaya).................. kata ..................kijiji............
4. Uraia ..........................................................................................
5. Shule ya msingi unayotoka........................................................
6. Dini (dhehebu) ............................................................................
7. Mahali unapoishi sasa ( *kwa mwanafunzi atakaye panga tu)*
   i. Jina la kitongoji ..........................................................................
   ii. Jina la mwenye nyumba ...........................................................
   iii. Jina la mwenyekiti wa kitongoji ................................................
8. a) Jina la mzazi / mlezi ..............................................................
   b) kazi ya mzazi / mlezi ...............................................................
   c) Anwani yake ...............................................................................
   *(Mabadiliko yote ya anwani yawasilishwe ofisini mara moja)*
   d) Namba yake ya simu ...................................................................
9. Ahadi ya mwanafunzi:

   Mimi ......................................... Nakubali/sikubali nafasi niliyopewa. Naahidi / siahidi kutii kikamilifu sheria na kanuni zote za shule na kuzitekeleza kinyume chake nichukuliwe hatua zinazostahili.

   Saini ......................................... Tarehe..................................

10. Ahadi ya mzazi/ mlezi:
   Mimi ............................................................ mzazi / mlezi wa ................................... nimeyasoma na kuyajadili na mwanagu maagizo haya. Nimeikubali nafasi hii aliyopewa mtoto wangu na Taifa. Nitamtimizia mahitaji yake yote bila usumbufu wowote. Aidha nitahakikisha kuwa muda wote anazingatia sheria na kanuni zote za shule.

   Saini ......................................................... Tarehe...................................

# MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING

## MSUVA SECONDARY SCHOOL

### STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION

*( To be completed by the Government Medical officer and return to the Headmaster, Msuva sec. school)*

- Student's full name: ...................................................................................
- Present age: ...........................................................................................
- Blood test: .............................................................................................
- Stool: .......................................................................................................
- T.B: ...........................................................................................................
- Asthma: ...................................................................................................
- Blood Pressure: ........................................................................................
- Sight: ........................................................................................................
- Hearing: ....................................................................................................
- Skin disease ..............................................................................................
- Operations: ...............................................................................................
- Serious Accidents: ....................................................................................
- Any other infection disease:.......................................................................
- Pregnancy: ................................................................................................
- Physical defects or impairment: ...............................................................

I certify that I have personally examined Mr. / Miss.................................. and found him / her fit / un fit to pursue with studies.
Signature:.......................................
Designation.....................................
Official rubber stamp.........................